

INSTRUCTIONS FOR SCHOLARSHIP APPLICANTS - please read carefully!
(MAELEKEZO KWA WAOMBAJI WA UFADHILI WA KUSOMA - soma kwa makini!)
TAFADHALI SOMA KWA MAKINI - FOMU YA MAOMBI NA IJAZWE KIKAMILIFU.

Maombi kwa ufadhili - ELIMU YA MSINGI

SHULE YA MSINGI:

- 1. Mzazi au Katibu wa Idara atajaza fomu ukurasa wa 1- taarifa ya msingi ya mwanafunzi / muombaji
- 2. Mzazi au Katibu wa Idara atajadiliana na mtoto katika kujibu maswali na kisha kumsaidia mtoto kujaza majibu.
- 3. Eleza tafadhali, kwa nini ufadhili unahitajika (kama ni shule binafsi - je, ni lazima?) Tafadhali eleza mazingira yanayo pelekea mtoto kuhitaji ufadhili huu

- 4. Mchungaji wa Ushirika atasaini fomu ya maombi (uk.1) na ataandika barua ya mapendekezo
- 5. Chukua picha ya fomu iliyojazwa kikamilifu PAMOJA na fomu hii ya maelekezo ikiwa imejibu swali la 3, na la 4 kama ilivyo hapo juu -

SHULE YA SEKONDARI:

- 1. Mzazi, Mwanafunzi au Katibu wa Idara atajaza fomu ukurasa wa 1- taarifa ya msingi ya mwanafunzi / muombaji.
- 2. Mwanafunzi ajibu maswali yaliyoko ukurasa wa 2 na asaini fomu. Katibu wa Idara anaweza kumsaidia mtoto katika kujibu maswali.
- 3. Wanafunzi wa Sekondari hawahitajiki kujibu maswali yaliyoko ukurasa wa 3
- 4. Mzazi au Mchungaji, tafadhali elezea ni mazingira gani yanayopelekea mwanafunzi huyu kuhitaji ufadhili. NB: Nafasi kama haitoshi, tumia karatasi nyingine kisha iambatanishe na fomu hii ya maombi.
- 5. Mchungaji wa Ushirika atasaini fomu ya maombi (uk.1) na ataandika barua ya mapendekezo
- 6. Chukua picha ya fomu iliyojazwa kikamilifu PAMOJA na fomu hii ya maelekezo ikiwa imejibu swali la 3, na la 4 kama ilivyo hapo juu -

Maombi kwa ufadhili - ELIMU NGAZI YA:-

CHETI, DIPLOMA, MASOMO YA UFUNDI STADI AU MAFUNZO YA UJUZI WA KUENDESHA MRADI :

- 1. Mwanafunzi au Katibu wa Idara atajaza fomu ukurasa wa 1- taarifa ya msingi ya mwanafunzi.
- 2. Mchungaji wa Ushirika atasaini fomu ya maombi (uk.1) na ataandika barua ya mapendekezo
- 3. Mwanafunzi ajibu maswali yaliyoko ukurasa wa 2 & 3 na asaini fomu.
Endapo muombaji hakumaliza elimu ya sekondari, basi anaweza kujibu maswali katika lugha yake mfano; kiSpaniola, ki Faransa ama kiswahili; ili mradi Katibu wa Idara atatoa tafsiri yake katika lugha ya Kiingereza.
- 4. Chukua picha ya: 1). Fomu iliyojazwa kikamilifu 2). Barua ya mapendekezo ya Mchungaji
3. Vyeti pamoja na alama za kuhitimu elimu ya nyuma kabla ya kujiendeleza katika ngazi hii nayoiombea ufadhili

CHUO KIKUU

- 1. Mwanafunzi atajaza fomu ukurasa wa 1- taarifa ya msingi ya mwanafunzi.
- 2. Mchungaji wa Ushirika atasaini fomu ya maombi (uk.1) na ataandika barua ya mapendekezo
- 3. Mwanafunzi ajibu maswali yaliyoko ukurasa wa 2 & 3 na asaini fomu.
Endapo nafasi haitoshi; tafadhali kuwa huru kuelezea zaidi kwenye karatasi nyingine, kisha ambatanishe na fomu yako ya maombi.
- 4. Chukua picha ya: 1) Fomu iliyojazwa kikamilifu 2) Barua ya mapendekezo ya Mchungaji
3) Vyeti pamoja na alama za kuhitimu (grades) elimu ya sekondari .

KISHA TUMA kwa:-

Dawati la Wanawake Duniani kwa - e mail hii: unitywomen2011@gmail.com

AU kwa WHATSAPP: +13365758577